وسائل الثبات - سواحيلي

# NYENZO ZA KUTHIBITI



جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

284

# NYENZO ZA KUTHIBITI

## وسائل الثبات - سواحيلي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
Tel: 966 164234466 - Fax: 966 164234477

# وسائل الثبات - سواحيلي

**أعده وترجمه للغة السواحيلية**

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**

**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**


ح جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ



***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
وسائل الثبات / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد
وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ

٤٠ ص ؛ ..سم

ردمك: ٤-١٩-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- الوعظ و الارشاد ٢- الفتن في الاسلام أ.العنوان

ديوي ٢١٣ ١٤٤٤/٥٨٣٢

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨٣٢**
**ردمك: ٤-١٩-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨**

# NYENZO ZA KUTHIBITI
# وسائل الثبات

## Utangulizi

Kila Sifa Njema Anastahiki Allah; tunamshukuru, tunamtaka msaada, tunamuomba msamaha na tunajilinda kwa Allah kutokana na shari zitokanazo na nafsi zetu, na (tunajilinda) na ubaya wa matendo yetu. Yoyote ambaye Allah amemuongoa, basi hakuna wa kumpoteza, na yoyote ambaye Allah atampoteza, basi hakuna wa kumuongoza. Na ninashuhudia kuwa hapana Mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Peke Yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammad ni Mja wake na ni Mtume wake.

Ama baada ya hayo, Kwa hakika kabisa miongoni mwa tabia za Muislamu wa kweli na kikubwa kinachompambanua ni kuthibiti (kuimarika) katika Dini Yake, na kuhifadhi tabia za Mtume wake Muhammad - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake. Na kumfuata bila kuyumba na kwenda kombo kutokana na utata utakaojitokeza, au tamaa isiyozuilika, au mtihani uliyoenea. Kwa hakika

kuyumba kati ya haki na batili na kuacha suna (mwenendo wa Mtume) iliyothibiti baada ya kujipamba nayo, si jambo linaloendana na watu wenye Imani. Bali ni miongoni mwa mambo ya Wanafiki na Makafiri ambao wamezungumzwa katika Qur'ani Tukufu, kuwa maneno yao yanapingana na matendo yao, na hujipinduapindua njiani katika hali zote. Allah Anasema: *"Na miongoni mwa watu wapo wanaomuabudu Allah upande mmoja tu, basi endapo atapata kheri anatulia kwa kheri hiyo na endapo fitna ikimpata anageuka na kuritadi (kutoka katika Dini yake), amekhasirika duniani na akhera na huko ni kukhasirika kuliko wazi mno."*[1]

Hakika ya kujikita katika njia ya haki na kuthibiti, ni miongoni mwa mambo muhimu ambayo Muumini anapaswa kuyachunga na ayafanyie kazi. Na mambo hayo mawili ni miongoni mwa neema kubwa ambazo, ni wajibu kwa mtu azishukuru na kuzihifadhi.

---

1. Sura Al Haji ( 22 ) Aya ya 11

Na kinachokusudiwa katika kujikita katika haki ni: Kushikamana na twaaa (utiifu) kwa Allah na kutekeleza kile alichokiamuru katika mambo ya wajibu, na kujiweka mbali na yote aliyoyaharamisha, na kuwa na *Istiqama* (msimamo) humo.

Imenukuliwa kutoka kwa Sufiani bin Abdillah Athaqafy amesema: “Nilisema: Ewe Mjumbe wa Allah niambie, kauli moja katika Uislamu sitamuuliza mwingine yoyote baada yako, akasema: *“Sema nimeamini Allah kisha kuwa na msimamo…”*

Katika Hadithi hii Mtume, Allah amshushie rehema na amani amemuamuru awe na msimamo, nako ni kwenda mwendo wa sawa usio na kupinda pinda au kwenda kinyume, na huko ndio kuwa na Msimamo hasa.

Hivyo basi, kushikamana maana yake: Ni kushika mana na Dini ya Allah, ndani na nje. Kushikamana katika itikadi, kushikamana katika ibada, kushikamana katika mienendo na tabia, kushikamana katika kuamiliana, huku ndiko kushikamana kulikokamilika.

Kushikamana na hayo katika kila mambo ya maisha. Kushikamana misikitini, kushikamana kazini, kushikamana sokoni, kushikamana nyumbani, kama ambavyo Allah Amesema: *"Sema, hakika Swala yangu na ibada yangu, na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika yeye, hivyo ndivyo nimeamrishwa na mimi ni Muislamu wa kwanza."*[2]

Na pale mja anapotubu na kushikamana na amri za Allah, basi kwa hakika atakuwa amejua kuwa yeye sasa amehama kutoka maisha fulani kwenda katika maisha mapya. Na kwa hakika yeye ameaga maisha ya kiholela, kucheza, maisha ya uasi na maisha kutojali na sasa bila shaka anaelekea kwa Allah. Basi inampasa aandae kwa ajili ya nafsi yake hali ya hewa itayoendana na maisha mapya na afanye mabadiliko katika mtiririko wa maisha yake.

Basi kitabu alichokuwa akikisoma anakibadili kwa kitabu cha Kiislamu, jarida alilokuwa akilisoma - nalo si la Kiislamu - anaaza kulibadili na kuanza kusoma jarida la Kiislamu, rekodi ya sauti aliyokuwa akiisikiliza, iwe ya mziki na nyinginezo

2. Sura al An'aam (6) Aya ya 161-162.

anaanza kuzibadilisha na kuanza kusikiliza rekodi za Kiislamu. Hivyo hivyo usingizi kama alikuwa anachelewa kulala anabadili anaanza kulala mapema ili awahi kuamka kwa ajili ya Swala ya al-Fajiri. Na Yule aliyekuwa rafiki na mwandani ambaye alikuwa anakwenda naye katika batili, anamuacha na anatafuta rafiki mwenza mwingine anayekwenda naye kwenye haki na kumsaidia katika haki na hivyo hivyo katika mambo mengine.

Kuthibiti katika Dini ya Allah ni takwa la msingi la kila Muislamu wa kweli. Muislamu anataka kupita njia iliyonyooka kwa azma na uelewa. Kawaida, pale inapokithiri mitihani na kuenea vishawishi, huongezeka wanaoanguka, na wanaorudi katika uovu. Wapo wanaoanguka kwa hofu na wapo wanaoanguka kwa tamaa, na miongoni mwao wapo wanaoanguka kwa kuto kujua.

Katika zama hizi ambazo uhalisia umebadilika na uwelewa umegeuka na mitihani imekuwa mingi, vishawishi vingi na njia za upotevu zimekuwa rahisi kufikika. Dunia inadanganya nafsi kwa neema zake zisizo za kudumu. Katika zama hizi uhitaji ulioje tulionao wa maelekezo ya Mtume yenye huruma! Maelekezo yanayomuweka mbali Muislamu na kila

aina ya upotofu mbaya na kwenda kombo. Pale Mtume aliposema: "...enyi waja wa Allah thibitini."[3]

Hakika ya kuthibiti mbele ya mambo mazito na mitihani, na mbele ya kugeuka geuka dunia na vishawishi vyake, ni alama miongoni mwa alama za waja wa Allah waliyoongoka. Waja wanaoelewa kuwa si vingine, hakika kuwepo kwa mitihani ni kwa ajili ya kuwasafisha Waumini. Na ni majaribu kwa walioghafilika wafanyao mchezo. Kundi lililoamini, imani yake haibadilishwi na matatizo (anayokutana nayo mtu). Bali matatizo yanamzidi - shia Imani na kukinai na kumthibitishia kuwa yupo katika njia salama na humuonesha umuhimu wa kuthibiti katika njia anayopita. Allah Anasema: *"Alif laam, miim. [Allah Ndiye Anajua maana ya herufi hizi mkato]. Hivi wanadhani watu wataachwa tu hivi hivi waseme tumeamini na bila wao kutahiniwa? Na kwa hakika Tuliwatahini wale waliyokuwa kabla yao, basi kwa hakika kabisa Allah Atawaelewa ambao wa kweli, na kwa hakika kabisa Atawaelewa ambao ni waongo."*[4]

---

3. Hadithi imenukuliwa na Imamu Muslim Allah Amrehemu.

4. Sura Al-Ankabuti (29) Aya ya 1-3.

Hakika kuthibiti maana yake, ni kule Muumini kuendelea kubaki katika njia ya uongofu na kushikamana nayo na kudumu katika amali za kheri. Na kufanya haraka hali ya kujitahidi ili kutaka ziada. Na siku zote anapupia kuwa leo yake iwe bora kuliko jana yake, na kesho yake iwe bora kuliko siku yake ya leo. Kila siku inayopita inamuweka karibu na Akhera. Kila mwanadamu hana budi kupita katika nyakati ambazo hamasa yake inapungua. Isipokuwa kwa Muumini huwa anapambana na nafsi yake na anakuwa na subira ya kudumisha amali njema na kushindana katika mambo yenye maslahi na yenye kumuokoa Siku ya Kiama. Allah Mtukufu Anasema: *"Enyi ambao mmeamini kuweni na subira, na shindaneni kusubiri, na shikamaneni na mcheni Allah ili muweze kufaulu."*[5]

Allah pia Anasema: *"Shindaneni kuyaendea maghufira toka kwa Mola wenu Mlezi na pepo upana wake, ni kama upana wa mbingu na ardhi…"*[6]

5. Sura Aali Imran (3) Aya ya 200.

6. Sura al-Hadidi (57) Aya ya 21.

Kwa hali yoyote mtu atavyochoka, lakini kuna hatua ambayo hatokubali kushuka au kuzembea chini ya hapo, hata kama mguu wake utateleza basi hatakaa muda mrefu atarudi na kutubu kwa Mola wake Mlezi.
Allah Mtukufu Ametaja katika Kitabu Chake Kitukufu aina mbali mbali za kuthibiti (kuimarika) katika maisha ya Muislamu. Na hilo si kwa sababu nyingine isipokuwa tu ametaka Muislamu ahisi umuhimu wa hii kadhia na atowe juhudi zake kurudi katika daraja la waliyomtangulia miongoni mwa Maswahaba na Taabiina. Na umuhimu wa *istiqama* na kuthibiti ndani ya Dini na amali njema unakuwa katika mambo yafuatayo:

Hali ya Jamii za sasa ambazo Waislamu wanaishi. Miongoni mwa jamii hizo, mtu anaishi katika aina mbali mbali za mitihani na vishawishi ambavyo moto wake unamchoma na kuna aina ya matamanio ambayo kwayo Dini kwake imekuwa ngeni na walioshikamana na Dini wamekuwa mfano wa ajabu. Kama alivyosema Mtume, Allah Amshushie rehema na amani, kwamba, *“Zitakuja zama kwa watu, yule ambaye atasubiri miongoni mwao katika*

*Dini yake, atakuwa sawa na aliyeshika kaa la moto."*[7]

Na hakuna mashaka yoyote kwa kila mwenye akili, kwamba mahitaji ya Muislamu wa leo ya nyenzo za kuthibiti na kuimarika ni makubwa sana kuliko yalivyokuwa mahitaji ya ndugu yake Muislamu katika enzi za wema waliotangulia. Jitihada inayohitajika ili kuhakikisha kuthibiti ni ya hali ya juu. Hilo ni kwa sababu ya kuharibika zama na kukosekana ndugu wa kweli wa kumsaidia katika kuishi Maisha ya kuthibiti katika Dini na uchache wa waunga mkono katika mambo ya kheri.

## Baadhi ya Nyenzo za Kuthibiti

Hakika miongoni mwa Rehema za Allah - Mtukufu - kwetu, ni kutubainishia katika Kitabu Chake, na katika ulimi wa Mtume wake - Allah Amshushie rehema na amani, na katika mwenendo wake, nyenzo nyingi za kuthibiti. Hapa tunazieleza baadhi ya hizo:

7. Hadithi imenukuliwa na Imamu Atirmidhy: 1844

**Ya kwanza:** Kuielekea Qur'ani Tukufu:

Hakika ya Qur'ani iliyotukuka ndio nyenzo ya kwanza ya kuthibiti (kuimarika Imani ya mtu). Yeyote atakayoshikamana nayo Allah Atamlinda na atakayoifuata Allah Atamuokoa, na atakayeilingania (atakayeitangaza) Allah Atamuongoza katika njia iliyonyooka.

Allah Ametaja kuwa lengo ambalo kwalo ameteremsha hii Qur'ani kidogo kidogo, ikipambanuliwa, ni kuthibiti. Allah - Mtukufu Amesema katika hali ya kuzijibu *shubha* (utata) za Makafiri: *"Na wakasema Makafiri kwa nini asingeteremshiwa yeye Qur'ani kwa pamoja mara moja, (Tumeiteremsha) hivyo ili kuithibitisha kifuani mwako na ndio Tumeisoma kwa mafungu. Na hawatakuletea mfano wowote isipokuwa na sisi Tutakuletea (jawabu) kwa haki na tafsiri nzuri."*[8]

Ni kwa Nini Qur'ani Imekuwa Nyenzo ya Kuthibiti?

- Sababu Qur'ani inapandikiza Imani (moyoni), na inakuza muunganiko wa mja na Mola wake Mlezi.

8. Sura Al-Furqani (25) Aya ya 32-33.

- Sababu Qur'ani inajibu shubha (utata) wanazozieneza maadui wa Uislamu miongoni mwa Makafiri na Wanafiki.
- Sababu inampa Muislamu misingi bora na mafundisho sahihi yanayomfanya kuelewa haki, na uhakika wa usalama wa njia anayopita.

## Ya pili: Elimu:

Yule anayetembea bila ya elimu, ni sawav na mfano wa yule anayetembea katika kiza; na yule anayetembea katika kiza ni sawa na anayetembea katika upeo wa macho na huenda anaweza kupata tatizo katika njia yake bila ya yeye kuhisi chochote. Basi hivyo hivyo mtu anayetembea bila ya elimu, ni rahisi kuingia katika vishawishi vya mambo yaliyo na utata na ya matamanio.

Ni lazima kwa mtafuta elimu achunge mambo yafuatayo:

- Kuitakasa nia yake kwa ajili ya Allah Pekee.
- Atie nia katika kutafuta kwake elimu kuondoa ujinga katika nafsi yake.

- Atie nia katika kutafuta kwake elimu kuondoa ujinga katika umma.
- Atie nia katika kutafuta kwake elimu kuhifadhi sheria ya Kiislamu na kuilinda (kuipambania).
- Atie nia katika kutafuta kwake elimu, kueneza itikadi sahihi ya Kiislamu

## Ya tatu: Kushikamana na sheria za Allah na amali njema:

Allah Mtukufu Amesema: *"Allah Huwafanya wawe imara wenye kuamini (kutamka) kauli thabiti katika maisha ya duniani na akhera na Allah Anawapoteza madhalimu na Allah Hufanya Atakacho."*[9]

Ama katika maisha ya dunia, basi Huwaimarisha kwa kutenda kheri na amali za kheri. Na akhera kwa maana ya kaburini Huwaimarisha kwa kujibu wanachouliza Malaika wawili kuhusu Mola wao Mlezi, Dini yao na Mtume wao, na watajibu sawa sawa.

Na Allah Mtukufu Amesema: *"Na lau kwa hakika wao wangefanya kile wanachowaidhiwa nacho,*

9. Sura Ibrahim (14) Aya ya 27.

*ingekuwa kheri kwao. Na (ingekuwa) kuthibiti kuliko kukubwa."*[10]

Kwa maana ya kuthibiti katika haki. Hili liko wazi, kama si hivyo je inawezekana kuthibiti mtu mvivu asiyetenda mema inapodhihiri fitna?! Lakini wale walioamini na wakatenda amali njema Mola wao Mlezi Atawaimarisha. Na kwa hivyo ndio maana Mtume - Allah Amshushie Rehema na Amani -, amesema, '*Allah - tendo Analolipenda zaidi ni lile linalodumu hata likiwa chache.*'

Ya nne: Kuzingatia simulizi za Mitume, na katika kuzisoma simulizi hizo ni kwa ajili ya kuiga na kutenda:

Ushahidi wa hilo ni Kauli Yake Allah Mtukufu: *"Na yote Tunayokusimulia ewe Muhammad, miongoni mwa habari za Mitume ya kabla yako ni ya kuupa nguvu moyo wako, na katika haya imekujia haki na mawaidha na ukumbusho kwa Waumini."*[11]

Hazikuteremka Aya hizi katika enzi za Mtume - Allah Amshushie Rehema na Amani - kwa mchezo

10. Sura Annisaa (4) Aya 66.

11 Sura Hudi (11) Aya 120

na kustarehe (zinaposomwa). Hakika si vingine zimeteremka kwa lengo kubwa. Lengo lenyewe ni kuuimarisha moyo wa Mtume wa Allah na kuimarisha nyoyo za Waumini pamoja naye.

## Ya tano: Duwaa:

Miongoni mwa sifa za waja wa Allah - Waumini, kwamba wao wanamuelekea Allah kwa kumuomba awathibitishe. Na dua ni moja ya sababu za kupata kuthibiti (kuimarika), na miongoni mwa dua ni: *"Ewe Mola wetu Mlezi Usizipindishe (usizipotoshe) nyoyo zetu baada ya kutuongoza."*[12] na *"Ewe Mola wetu Mlezi Tuingizie sisi subira na Zithibitishe nyoyo zetu..."*[13]

Na kwa hakika Mtume wa Allah, Allah Amshushie rehema na amani - alikuwa anakithirisha katika dua zake kwa kusema: "*Ewe Mwenye kuzigeuza geuza nyoyo Uthibitishe moyo wangu katika Dini Yako."*[14]

## Ya sita: Kumtaja Allah:

Hakika kumtaja Allah ni miongoni mwa njia zilizo na manufaa Zaidi. Pale ilipokuwa suala la kumtaja

12. Sura Aali Imran (3) Aya ya 8.

13. Sura al-Baqara (2) Aya ya 250.

14. Hadithi imenukuliwa na Imamu Atirmidhy.

Allah lina athari kubwa ndani ya nafsi ya Muumini katika kupandisha morali. Hiyo ni kwa sababu mtu anapomtaja Allah anakuwa na mafungamano na nguvu isiyoshindwa.

Ya saba: Muislamu kupupia kupita njia sahihi: Na hili linapatikana kwa kufahamu Dini ufahamu sahihi. Na ataupata ufahamu huu katika Kitabu na suna za Mtume - Allah Amshushie rehema na amani. Muislamu atahadhari na fikra potofu na itikadi zisizo sahihi. Mtume - Allah Amshushie rehema na amani- anasema katika Hadithi iliyopokelewa na Arbadhi bin Saria: *"... hakika yake atakayeishi muda mrefu miongoni mwenu baada yangu, basi ataona tofauti nyingi, na juu yenu kuzishika suna zangu na suna za Makhalifa wangu viongozi. Shikamaneni nazo na zing'ateni kwa magego. Na jiepusheni na mambo ya uzushi, kwa hakika kila uzushi katika Dini ni bidaa (uzushi) na kila uzushi ni upotofu."*[15]

## Ya nane: Malezi:

Malezi ya kiimani na kielimu. Ufahamu wa kidogo kidogo ni nyenzo ya msingi katika nyenzo za

15. Hadithi imenukuliwa na Imamu Ahmad, Abu Daudi, Tirmidhy na Ibn Maaja katika vitabu vyao kwa sanadi zilizo sahihi.

kuthibiti. Hayo ndio malezi yanayohuisha moyo na dhamira kwa - kuogopa, matarajio na mahaba kwa ajili ya Allah.

**Malezi ya kielimu:**
Malezi yanayosimama kwa dalili sahihi zinazopinga -na na kuiga na kufuata bila ya hoja.

**Malezi ya uwelewa:**
Malezi ambayo hayapiti njia ya waovu. Malezi ya kuisoma mikakati ya maadui wa Uislamu na kuufahamu uhalisia wake.

**Malezi ya hatua kwa hatua:**
Malezi ambayo yanamuendesha Muislamu kidogo kidogo kulingana na uwezo wake (kimwili na mali). Malezi ambayo yanapingana na kufanya mambo bila ya maandalizi au kuwa na uharaka usiyo na maandalizi na michupo inayobomoa.

Waislamu ni lazima kujali masuala ya malezi tangu utoto. Kwa hakika vijana wanabeba nafsi zenye rutuba na nyoyo zilizo safi. Ni rahisi wanapokuwa katika hali hiyo kuwabebesha tabia nzuri na sifa nzuri. Kwa sharti hayo malezi yawiane na mahitaji

ya nafsi ya mwanadamu. Kuipatia mahitaji yake bila kuzidisha au kupunguza.

Na ili tujue umuhimu wa kipengele hiki katika nyenzo za kuthibiti, basi turudi kwenye mwenendo wa Mtume - Allah Amshushie rehema na amani - na tuziulize nafsi zetu, ni lipi chimbuko la kuthibiti kwa Maswahaba wa Mtume - Allah Awaridhie? Walipo-kuwa katika mji wa Makkah, wakati wa mateso. Hivi yawezekana kuwa kuthibiti kwao hakukutokana na malezi thabiti yatokanayo na taa (muongozo) ya Mtume?

Basi tumchukuwe Swahaba mfano wa Khabbabu bin al-Aratti - Allah Amridhie - ambaye bwana wake anayemmiliki, alikuwa anaweka chuma kwenye moto mpaka kinakuwa chekundu kisha anamtupia mgongoni, ukiwa hauna nguo, na hakizimi chuma hicho isipokuwa huzimwa na mafuta ya mgongo wa Khabbab, yakichuruzika kwenye hicho chuma. Kipi kilichompa subira ya kuvumilia hali hii yote?

Na (Swahaba) Bilali bin Rabaah - Allah Amridhie - ni nini kilimfanya athibiti chini ya jiwe kwenye joto kali, akiwa katika adhabu kali?

Na mwingine ni Sumaiyya, mwanawe na mumewe. Ni nini kimewafanya wathibiti na kutotetereka pamoja na adhabu kali waliyoipata (kutoka kwa makafiri)? Kama kusingekuwa na malezi ya kweli yaliyothibitisha na kuikitisha imani ndani ya nafsi zao.

## Ya tisa: kuiamini njia:

Hapana shaka yoyote kwamba kila panapozidi suala la kuamini usahihi wa njia ambayo Muislamu anapita, inakuwa kuthibiti katika hilo ni kukubwa. Na katika hili kuna njia nyingi, miongoni mwa hizo ni:

- Kuihisi njia iliyonyooka unayoipita. Hakika wamepita humo kabla yako Mitume, wakweli, Wanawazuoni, Mashahidi na Waja wema. Basi hapo ugeni wako unakuondoka, upweke wako unageuka kuwa liwazo, huzuni yako inageuka kuwa furaha. Kwa sababu unahisi kwamba hao wote ni ndugu kwako katika njia na mfumo.
- Hisia za kuchaguliwa na Allah. Allah Mtukufu Anasema: *"Kila Sifa Njema ni za Allah, na amani iwe juu ya waja wake ambao Amewachagua..."*[16]

16. Sura Annamli (27) Aya ya 59.

- Hivi zingekuwaje hisia zako kama Allah Angekuumba kafiri mkaidi, au mlinganiaji wa bidaa (uzushi) au ungekuwa fasiki (muovu).
- Hivi huoni hisia zako kwa vile Allah kakuchagua, na Akakufanya kuwa katika mfumo wa haki. Unafuata yale aliyokuwa nayo Mtume - Allah Amshushie rehema na amani -, na Maswahaba zake, kuwa ni miongoni mwa nyenzo za kuthibiti kwako katika mfumo wako na njia yako?

## Ya kumi: Kufanya daawa kuelekea kwa Allah Mtukufu:

Hakika ya daawa ya Allah ni miongoni mwa Nyanja za kuizindua nafsi. Huo ni wadhifa wa Mitume, nafsi kama haikuchangamka inasimama, na kama hukuishughulisha na utiifu itakushughulisha kwa maasi. Imani inazidi na kupungua, inazidi kwa kutii, na inapungua kwa maasi.

Hivyo daawa - pamoja na malipo yake makubwa - pia ni nyenzo miongoni mwa nyenzo za kuthibiti (kuimarika). Kwa hakika anayeshambulia haitaji ulinzi na Allah yuko pamoja na Walinganiaji anawathibitisha na kuwafutia makosa yao. Na Mlinganiaji ni kama daktari anapambana na maradhi kwa uzoefu wake na elimu aliyo nayo.

Kama ilivyo kwamba kuna malipo maalumu juu ya kazi hii kubwa, Allah Mtukufu Anasema: *"Hivi ni nani aliye na kauli nzuri, kuliko yule anayelingania kwa Allah na akatenda amali njema, na akasema hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu."*[17]

Mtume - Allah Amshushie rehema na amani - anasema: *"Allah Akikuwafikisha kumuongoa mtu mmoja tu ni kheri kwako kuliko kumiliki ngamia wekundu."*[18]

Ya kumi na moja: Kuzunguka pembezoni mwa vitu vilivyothibitisha (vinavyoimarisha):
Hivyo ni miongoni mwa vitu ambavyo sifa zake ni zile alizotueleza Mtume - Allah Amshushie rehema na amani-, aliposema, *"Hakika miongoni mwa watu kuna watu (ambao ni) funguo kwa ajili ya kheri, (na) vifungio vya shari."* [19]

Na kuwatafuta Wanazuoni wa kweli, na ndugu wenye nasaha na kuwa nao karibu pembezoni mwao ni sababu muhimu miongoni mwa sababu za

17. Sura Fuswilat (41) Aya ya 33.

18. Hadithi imenukuliwa na Imamu Bukhary (3009)

19. Hadithi imenukuliwa na Imamu Ibnu Maajah kutoka kwa Anasi 194.

kuthibiti. Basi ndugu zako walio wema, ni viigizo na walezi (wazuri). Hao ndio msaada kwako - baada ya Allah - unapokuwa njiani. Wanakuimarisha kwa waliyokuwa nayo katika Aya za Allah na hekima. Jilazimu kuwa nao na ishi pamoja nao, na usiinyime nafsi yako fadhila za vikazi vya dhikri (kumtukuza Allah). Na jiepushe na upweke usije ukaporwa na mashetani. Kwa hakika mbwa mwitu hula mbuzi aliyejitenga mbali na wenziwe.

Ya kumi na mbili: Kuwa na imani juu ya kupata msaada wa Allah, na kwamba mustakabali (mzuri) ni wa Uislamu:

Allah Mtukufu Anasema: *"Enyi ambao mlio amini, ikiwa mtamnusuru Allah; Atakunusuruni na atazithibitisha nyayo zenu."* [20]

Allah Mtukufu Anasema: *"Hakika Allah Anawalinda wale ambao wameamini..."*[21] na Anasema, *"...Allah ni walii (Msimamizi) wa wale ambao walio amini..."*[22]

---

20. Sura Muhammad (47) Aya ya 7.

21. Sura al-Hajji (22) Aya ya 38.

22. Sura al-Baqara (2) Aya ya 257.

Ya kumi na tatu: Kujua uhakika wa batili na kutodanganyika nayo:
Na katika Kauli ya Allah - Mtukufu - Amesema, *"kabisa kusikudanganye kutangatanga kwa wale ambao wamekufuru katika miji. Ni starehe ndogo kisha mafikio yao ni moto wa Jehanamu na ubaya wa mafikio ni huo."* [23]

Huku ni kuwazindua Waumini kuwa wasighurike na mambo waliyo nayo Watu wa batili na mambo ambayo mara nyingi wanayapata. Na yale ambayo watakayoweza kuyafikia wakiwa katika nafasi za juu. Ya kwamba vyovyote itakavyokuwa mwisho wao ni moto wa Jehanamu na ubaya wa mafikio ni huo. Na haikuwa starehe ya dunia isipokuwa ni ya muda mfupi tu na inakwisha. Na haina thamani na hailingani hata kidogo na yale aliyowaandalia Allah Waumini - wenye sifa ya ukweli huko peponi.

## Ya kumi na nne: kujipamba na tabia zinazosaidia kuthibiti:

Na hizi zinaongozwa na subira. Katika Hadithi sahihi Mtume anasema: *"Na hakumpa mtu yoyote*

23. Sura Aali Imran (3) Aya ya 196.

*kitu cha kheri na kikubwa zaidi kuliko subira."*[24]

**Ya kumi na tano: Wosia wa mtu mwema**:
Fanya pupa ewe ndugu Muislamu mtukufu juu ya kutafuta wosia kutoka kwa watu wema, na uuzingatie pindi usomewapo wosia huo.

- Uombe wosia kabla ya kusafiri pale unapohofia kile kitakachotokea huko.
- Uombe wosia wakati wa majaribu, au kabla ya janga linalotarajiwa kutokea.
- Omba wosia pale unapoteuliwa katika nafasi fulani au ukiwa umerithi mali na utajiri.

Na ithibitishe nafsi yako, na mthibitishe mwenzako na Allah ni Msimamizi wa Waumini.

Ya kumi na sita: Kutafakari kuhusu neema za peponi na adhabu za motoni na kukumbuka umauti:

Pepo ni miji ya furaha, kiliwazo cha huzuni, mafikio ya safari ya Waumini. Na nafsi imeumbwa katika hali ya kutotaka kujitoa kwa kufanya juhudi, kutofanya amali na kutothibiti. Isipokuwa tu kwa kupata kinachorahisisha mambo magumu (kuwa

24. Hadithi imenukuliwa na Imamu Muslim (2471)

mepesi) na kuyafanya mepesi yaliyo njiani miongoni mwa vikwazo na tabu.

Basi yule anayejua kuwa kuna malipo, taabu zote huwa rahisi kwake. Huku anakwenda anajua kwamba endapo hatathibiti, pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, ataikosa.

Kama ilivyo suala la kukumbuka umauti Muislamu linamuhami katika kurudia kwenye maovu, na linamsimamisha katika mipaka ya Allah na hivyo kumfanya kutoyakiuka. Kwani mtu atakapojua muda wa kifo chake kuwa ni baada ya muda mchache, basi vipi nafsi yake itamshawishi apotee, au kuendelea katika kupotoka. Kwa sababu hii Mtume wa Allah amesema: *"Kithirisheni kukumbuka kikatacho ladha."* Kwa maana ya umauti.[25]

## Mawanda (Maeneo) ya Kuthibiti (Kuimarika)

Ya kwanza: kuthibiti katika mitihani:

Kwani katika sura za kuthibiti katika Dini, ni kuthibiti katika mitihani. Kuthibiti katika siku za subira ambayo atakayesubiri hapo atastahiki malipo

25. Hadithi imenukuliwa na Imamu Tirmidhy (2307).

ya Maswahaba hamsini. Kulingana na hali aliyo nayo ya kheri nyingi pale alipothibiti na kuvumilia wakati wa Fitina. Katika hili Mtume - Allah Amshushie rehema na amani - amesema, *“Hakika mbele yenu kuna masiku ya subira, kwa atakayeshikamana ndani yake, katika siku hiyo, kwa kile mlichonacho nyinyi atalipwa ujira sawa na watu hamsini miongoni mwenu.’ Wakasema, ‘ewe Nabii wa Allah: hivi nasi ni katika wao?’ Akasema: ‘ndio ni Katika nyinyi.”* [26]

## Miongoni mwa Aina ya Mitihani:

- Mtihani wa mali, na mtihani wa jaha:

  Na kutokana na uhatari wa mitihani hii miwili iliyopita, Mtume, Allah amshushie rehema na amani - amesema, *“Mbwa mwitu wawili wenye njaa walioachiwa kwa mbuzi, si waharibifu zaidi kuliko (uharibifu unaofanywa na) pupa ya mtu katika mali na utukufu katika Dini yake.”*[27] maana yake ni kuwa kupupia mali na Jaha kunaharibu zaidi Dini ya mtu kuliko uharibifu

26. Hadithi ipo katika kitabu cha silsila ya Hadithi sahihi cha Shekh Albany: 494.

27. Sahihi Atirmidhy (1935).

unaofanywa na mbwa mwitu wawili wenye njaa wakaachiwa kwenye Kondoo.

- Mtihani wa mke na watoto:
  Allah Mtukufu Anasema: *"...hakika wake zenu na watoto wenu ni maadui kwenu, jihadharini nao."*[28]

- Fitina ya mateso na dhuluma:
  Dhuluma iliyopindukia na majaribio ya kumzuia Muislamu kuitekeleza Dini yake.

- Mtihani wa Masihi Al-Dajali:
  Mtume - Allah Amshushie rehema na amani-, ametuhadharisha na mtihani wa Masihi Al-Dajali, na ametuamuru kuwa endapo tutatahiniwa naye tusubiri na kuthibiti, na kutoshawishika kwa atakavyokuwa navyo miongoni mwa madh-hari ya nguvu ya uchumi. Basi kwa hakika Mtume - Allah Amshushie rehema na amani - amesema: *"Na yeyote atakayekutana naye basi asome Aya*

28. Sura At-taghabun (64) Aya 14

*za mwanzoni mwa sura Al-Kahfi, hakika yeye atatokea eneo la (Khulat) kati ya Shamu na Iraq, ataharibu kulia na kushoto, enyi waja wa Allah thibitini."* [29]

- Na kwa hakika Mtume - Allah Amshushie rehema na amani, ametutajia mfano wa kuthibiti huko, wakati alipotupa habari ya kweli kuhusu Mtu Muumini anathibiti mbele ya mtihani wa Al Dajali, na kuwa na yakini ndio maandalizi yake katika huko kuthibiti. Imekuja katika Bukhary: *"Atakuja Dajali - naye ni haramu kwake kuingia njia za Madinah. Atafikia baadhi ya maeneo kame ambayo yapo Madinah, na atamtokea mtu bora wa zama hizo au miongoni mwa wa watu wa kheri wa wakati huo, atasema: 'Nashuhudia kuwa wewe ni Al-Dajali ambaye ametuhadithia Mtume, Allah Amshushie rehema na amani, kuhusu wewe." Basi Al-Dajali atasema, "waonaje kama nitamuua huyu kisha nimuhuishe, hivi mtakuwa na shaka na jambo langu?" Na*

29. Hadithi ameinukuu Ibnu Maajah (3294) kutoka katika Hadithi Nawasi bin Samaan.

*watasema: 'hapana.' Basi atamuua kisha anamuhuisha na atasema (Yule Mtu wa kheri) wakati anamuhuisha: 'Naapa kwa Allah kamwe hukuwa mwenye uoni mkubwa kuliko mimi leo.' Na Al-Dajali atasema, 'ninamuua.' Na hatokuwa na uwezo wa (kumuua).*" [30]

## Ya pili: Kuthibiti katika Jihadi:

Hakika ya Waumini walio wa kweli haziwazidishii sauti za panga na shida za umauti katika mapambano na wingi wa farasi wa maadui wa Allah isipokuwa huwazidishia kuthibiti na kujitoa Zaidi. Na kujitoa mbele ya Aliye Mmoja na Pekee (Allah), wakitaraji Msaada Wake, nyongeza na Msamaha toka Kwake, Allah Mtukufu Anasema: *"Ni Mitume wengi waliyotangulia walipambana wakiwa na kundi kubwa la maswahaba zao na hawakudhoofika kwa majeraha waliyoyapata kwa sababu hilo ni katika njia ya kupigania njia ya Mola wao Mlezi, na hawakushindwa na hawakusalenda kwa maadui zao. Hakika walisubiri kwa yale waliyoyapata na Allah Anawapenda wenye kusubiri. Na haikuwa kauli yao isipokuwa walisema: 'Ewe Mola wetu Mlezi tusamehe sisi dhambi zetu na yale tuliyoyafanya*

30. Imenukuliwa na Imamu Bukhary: 1882.

*katika kukiuka Amri za Allah na Ututhibitishe nyao zetu na Utunusuru juu ya watu Wadhalimu."*[31]

Hivi ndivyo walivyo watu wa msimamo, hawayumbishwi wala hawapeperushwi na vimbunga (Fitina) kama ambavyo vinavyopeperusha wengine miongoni mwa watu wa imani dhaifu. Allah Mtukufu Anasema: *"Na pindi walipotokeza kwa Jaluti na jeshi lake walisema: 'ewe Mola wetu Mlezi tupe sisi subira na Uzithibitishe nyao zetu na Utunusuru juu ya watu Makafiri."*[32] Hivyo yanakua matokeo ya hiyo subira ni kupata furaha Duniani, pamoja na yale wanayoyasubiri miongoni mwa malipo mazuri Akhera.

## Ya tatu: kuthibiti katika njia (Manhaji):

Hakika Muislamu wa kweli ni yule anayepupia kila aina ya pupa katika utekelezaji wa mafunzo ya Kiislamu. Pia anapupa katika kuacha uzushi (bidaa), maasi na upuuzi. Muislamu anashikamana na mwenendo sahihi hadi kufikia kuwa miongoni mwa watu walioongoka kwa Idhini ya Allah Mtukufu. Walinganiaji wa mambo ya bidaa ni wengi sana,

31. Sura Aali Imran (3) Aya ya 146-147.

32. Sura Al-Baqara (2) Aya ya 250

hasa katika zama za leo, kwani wao bidaa wameiingiza katika sheria za Allah. Na hawataki kujua kuwa sheria ya Allah imekamilika na haina mapungufu. Hivyo basi, ni wajibu kwa Muislamu kujihadhari na kuingiza bidaa katika Dini.

## Ya tano: Kuthibiti wakati wa kifo:

Hakika Makafiri na waovu wananyimwa ithibati katika nyakati za matatizo mazito. Wanashindwa kutamka shahada wakati wa kufa. Na hii ni katika alama ya mwisho mbaya. Kwa hakika Mtume - Allah Amshushie rehema na amani - amesema: *"Yeyote atakayekuwa mwisho wa maneno yake kauli ya 'la ilaha ila llah' ataingia peponi."*[33] Kwa maana hakuna Mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah. Hapati uwezo wa kuitamka kauli hiyo isipokuwa tu aliye Muumini aliye mkweli.

Na katika ishara za mwisho mbaya: Aliambiwa bwana mmoja wakati wa kifo chake: Sema *"Laa ilaha ila llah"* akawa anatikisa kichwa chake kulia na kushoto akikataa kusema.

33 Imenukuliwa na Imamu abu Daudi: (2673)

Na mwingine anasema wakati wa kifo chake: “Hiki kipande kizuri, hii bidhaa ni rahisi. Na wa tatu anataja majina ya sehemu za mchezo wa Bao. Na wa nne anaimba na kutamka maneno ya nyimbo au kumtaja mpenzi wake. Hii ni kwa sababu mambo hayo yamewashughulisha na hivyo kuacha dhikri ya Allah na kumuabudu, hawakuwafikishwa (kupewa uwezo) kuitamka shahada. Na huenda watu hawa zikaonekana sura zao kuwa ni nyeusi au wakawa na harufu mbaya, au kugeuzwa kutoka upande wa Kibla wakati wa kutoka roho zao. Na hakuna hila wala nguvu ya kuepukana na hayo isipokuwa ni za Allah tu.

Ama watu wema na watu wa suna (mwenendo sahihi), kwa hakika Allah Anawapa uwezo wa kuthibiti wakati wa kufa, na wanatamka shahada mbili. Huonekana katika hali zao kile kinachoashiria mwisho mwema, huonekana katika nyuso zao bashasha au harufu nzuri na aina ya bishara wakati wa kutoka roho zao. Kiasi kwamba Malaika wanawabashiria pepo.

Na mfano wa watu hawa, Allah Amewazungumzia kwa Kusema: *“Hakika wale ambao walisema Mola wetu Mlezi ni Allah, kisha wakasimama imara,*

*huteremka kwao Malaika wakisema: msiogope na msihuzunike na furahini kwa pepo ambayo mlikuwa mnaahidiwa."* [34]

Tafsiri ya Aya, *"Hakika wale ambao walisema Mola wetu Mlezi ni Allah, kisha wakasimama imara...*" katika tauhidi na mengine katika yale yaliyo wajibu kwao *"...huteremka kwao Malaika..."* wakati wa kufa, "*...msiogope…*" kifo na kitakachokuja baada yake, *"...na msihuzunike..."* kwa mlichokiacha, wake na watoto Sisi Tutawapa m-badala *"...na furahini kwa pepo ambayo mlikuwa mnaahidiwa*."

## Miongoni mwa Sura za Kuthibiti:

Bilali bin Rabaah: Bilali ni Mtumwa wa kihabeshi, mtoa Adhana wa kwanza wa Mtume, Allah Amridhie, naye awe radhi. Mtumwa huyu anamsikia Muhammad - Rehema na Amani ziwe juu yake - na daawa yake, na anakwenda haraka kuingia katika Dini ya Allah. Na kwa haraka bwana wake Umaiyya bin Khalaf anasikia habari za kusilimu kwake. Basi anafura kwa ghadhabu, na anaanza kumuadhibu ili kumrudisha kutoka kwenye Uislamu. Anapigwa

34. Sura Fuswilat (41) Aya ya 30

pigo kubwa, anatupwa juani bila maji wala chakula. yanawekwa mawe makubwa kifuani pake, naye anakariri kwa kusema mmoja, mmoja. Kila adhabu ilipozidi alizidisha kukariri wito huu wa milele. Adhabu iliendelea hadi alichoka bwana wake kuendelea katika hilo na Bilali akashika msimamo wake juu ya Uislamu wake. Anakuja Abubakari kwa bwana wa Bilali na anapatana naye hadi akamnunua kutoka kwake kisha anamuacha huru.

Katika vita ya Badri wanakutana Bilali na Umaiyya bin Khalaf, ambaye amemuadhibu kwa muda mrefu, ili aritadi (aachane na dini yake) mwisho inakuwa mauaji ya Umaiyya huyu katika mikono ya bilali mwenyewe.

Ammar bin Yasir: Baba yake asili yake ametokea Yemen, na ameishi Makkah, na akaoa mwanamke anaitwa Sumaiyya binti Khayyatu. Allah akawaruzuku mtoto wa kiume Ammar. Familia hii ndogo iliharakisha kuingia katika Uislamu, basi wakakumbana na maudhi makali toka kwa Makureishi (kabila kubwa pale Makkah). Hakika waliadhibiwa adhabu kali, kwa ajili ya kuwazuia wasifuate dini yao, na waliwekwa katika jua linalounguza katika jangwa la Makkah. Bila kupewa maji wala chakula,

ngozi zao ziliumizwa vibaya kwa fimbo, na waliwekewa vifuani mwao mawe makubwa. Na mama aliuliwa chini ya mapambano ya adhabu, ili awe shahidi wa kwanza katika Uislamu. Baba na mtoto walisubiri, na kuvumilia mateso haya kutoka kwa hawa Makafiri. Hivyo hawakuwa na jambo lingine baada ya kuona kuthibiti na kuvumilia kwao isipokuwa ni kuwaacha tu, baada ya kufeli mpango wao. Mtume - Allah Amshushie rehema na amani - alikuwa anampenda sana Ammar mapenzi ya hali ya juu, kutokana na ukweli wake na nguvu ya imani yake aliyoiona na msimamo wake katika haki.

Mus-abu bin Umair: Ni kijana aliye na uzuri wa hali ya juu na utajiri, aliyeishi maisha ya neema na raha. Mus-abu alisikia kile wanachokizungumzia watu wa Makkah kuhusu Muhammad al-Amini. Muhammad ambaye anasema kuwa Allah Amemtuma kuwa mlinganiaji kwenda kwenye ibada ya Allah Peke Yake na kuacha ibada zote zisizokuwa za Allah. Pia amesikia kuwa hakika Muhammad - Allah Amshushie rehema na amani - anakutana na Maswahaba wake katika nyumba ya al-Arqam bin Abi al-Aarqam akiwasomea Qur'ani na anawafundisha dini yao mpya. Alipanga jioni moja awaendee ili ajue kile anachokilingania Mtume

huyu. Punde tu aliposikia Aya za Qur'ani, Imani iliingia moyoni mwake, na akaamua kusilimu. Lakini aliamua kuficha Uislamu wake si kwa kuwaogopa Makureish, bali ni kumuogopa mama yake ambaye alikuwa anampenda sana, na alikuwa anamheshimu heshima ya hali ya juu. Mus-abu aliendelea kurudi mara kwa mara kwa Mtume - Allah Amshushie rehema na amani, na Maswahaba wake katika nyumba ya al-Arqam. Lakini mmoja wa Washirikina alimuona mara moja anaingia katika nyumba ile, basi haraka akaenda kumweleza mama yake Mus-abu. Na mrejesho wa tukio hili mama yake Mus-abu hakuwa na lingine isipokuwa alimfungia katika chumba kati ya vyumba vya nyumbani kwao, akijaribu kumlazimisha kutoka kwenye Dini ya Uislamu. Isipokuwa Mus-abu aliendelea kushikamana na Dini yake. Kisha baada ya kukimbia kutoka pale kifungoni, mama yake alimzuilia kila kitu, mavazi, chakula na mali. Kijana wa kitajiri akageuka fakiri, anavaa nguo zenye viraka na zilizochanika. Alijaribu kijana huyu mwema kumlingania mama yake kwenye Uislamu isipokuwa alikataa, na akaapa kamwe hataingia katika Dini hii. Na kutokana na nafasi kubwa aliyonayo Mus-abu kwa Mtume, Allah Amshushie rehema na amani, alimpeleka Madinah

ili awe mlinganiaji, kuwalingania watu wa Madinah na kuwafundisha Uislamu.

Na wakati alipofika hakukuwa na Waislamu isipokuwa kumi na wawili tu, lakini baada ya miezi michache walimuitikia watu wa Madinah wote kwa Fadhila za Allah.

Na katika vita ya Uhudi kijana huyu shujaa, anapambana mapambano ya kishujaa. Akiwa amebeba bendera ya Waislamu mkononi, na upanga katika mkono mwingine. Na wakamkusanyikia Washirikina, mmoja wa Washirikina alimpiga kwa upanga mkono wake, mkono ukakatika, bendera akaichukua kwa mkono mwingine na anaendelea kujilinda mwenyewe. Yule mshirikina akampiga na kuukata mkono mwingine, lakini huyu shupavu anakusanya nguvu zake na kuendelea kuibeba bendera kwa sehemu zake zilizobaki za mkono. Yule mshirikina anampiga mkuki kifuani pake na anaanguka Musabu bin Umair akiwa amekufa shahidi. Na bendera inaanguka chini hali ya kuwa Mtume - Allah Amshushie rehema na amani - anamuona, basi akasoma Kauli Yake Allah Mtukufu: *“Miongoni mwa Waumini kuna watu wametimiza yale*

*waliyoahidi kwa Allah ...”* [35]

Ummu Shariyk Ghaziyyatu binti Jabir: Jamaa wa mumewe walipojua kuwa amesilimu, walisema: tunaapa tutakuadhibu adhabu kali, Ghaziyyat anasema: ‘Waliondoka nami kutoka kwenye nyumba yetu, wakanibeba juu ya ngamia mbaya zaidi kati ya Ngamia wao na asiyekubali amri, wakinilisha mkate na asali, bila ya kunipa tone la maji hadi ilipofika kati kati ya mchana na jua likakoa, nasi tukiwa na kiu. Waliteremka wakaweka mahema yao wakania-cha juani, hadi nikatokwa na akili, usikivu na uoni. Walinifanyia hivyo kwa siku tatu, siku ya tatu wakaniambia: ‘Acha hiyo Dini uliyonayo.’ Akasema: ‘Sikuwa najua wanachosema isipokuwa neno moja moja tu, basi nawaashiria kwa kidole changu mbinguni (kwa kumpwekesha Allah) Tauhidi.’ Akasema: ‘Naapa hakika nilipokuwa katika hali hiyo, taabu imenishika, ghafla nilihisi ubaridi wa ndoo kifuani mwangu nikachukua nikanywa kwa pumzi moja. Kisha ikaondoshwa kwangu, nikawa naitazama. Nikaona inaning’inia kati ya mbingu na ardhi. Sikuweza (kuirejesha). Kisha ikateremshwa mara nyingine nikanywa kwa

35. Sura al-Ahzaab (33) Aya ya 23

mkupuo kisha ikaondoshwa. Nikaangalia nikaiona kati ya mbingu na ardhi. Kisha ikateremshwa mara ya tatu. Nikanywa humo hadi nikatosheka na nikamwagia kichwani mwangu na usoni mwangu na nguo zangu." Akaendelea kusema: "Wakatoka wakatazama wakasema umeyapata wapi maji haya ewe adui wa Allah?" Akasema: Nikawaambia; "hakika ya maadui wa Allah ni wale wasiokuwa mimi, sababu wamekwenda kinyume na Dini yake, ama swali lenu nimepata wapi haya maji? Basi ni kutoka kwa Allah, ni Riziki Ameniruzuku Allah." Akasema: "Basi wakaondoka haraka kwenye vyombo vyao wakakuta hakuna kilichofunguliwa." Wakasema kuwa tunashuhudia kwamba: "Hakika ya Mola wako Mlezi ndio Mola wetu, na kwamba Yule Aliyekuruzuku katika eneo hili baada ya kukufanyia yote haya tuliyofanya, Ndiye Aliyeleta Uislamu." Wakasilimu, na wakahama wote kwenda kwa Mtume wa Allah - Allah Amshushie rehema na amani-, na walikuwa wanachunga fadhila zangu kwao na Alichokifanya Allah kwangu.

Ewe Allah hakika sisi tunakuomba thabati katika Dini, na mwisho wa maombi yetu ni kuwa kila Sifa Njema anastahiki Allah Mola wa viumbe wote.
Na tunamshukuru Allah Ambaye kwa Neema Zake yanatimia mambo mema.

# Faharisi ya Kitabu

Utangulizi....................................................3
Baadhi ya Nyenzo za Kuthibiti ....................... 11
Ya kwanza: ................................................ 12
Ni kwa Nini Qur'ani Imekuwa Nyenzo ya Kuthibiti?
............................................................... 12
Ya pili: Elimu:........................................... 13
Ya tatu: Kushikamana na sheria za Allah na amali njema: ............................................. 14
Ya nne: Kuzingatia simulizi za Mitume, na katika kuzisoma simulizi hizo ni kwa ajili ya kuiga na kutenda:..................................................... 15
Ya tano: Duwaa:........................................ 16
Ya sita: Kumtaja Allah:.............................. 16
Ya saba: Muislamu kupupia kupita njia sahihi:.... 17
Ya nane: Malezi:........................................ 17
Malezi ya kielimu: ...................................... 18
Malezi ya uwelewa:.................................... 18
Malezi ya hatua kwa hatua: ........................ 18
Ya tisa: kuiamini njia:................................ 20
Ya kumi: Kufanya daawa kuelekea kwa Allah Mtukufu:................................................. 21
Ya kumi na moja: Kuzunguka pembezoni mwa vitu vilivyothibitisha (vinavyoimarisha):.................. 22

Ya kumi na mbili: .......................................... 23
Ya kumi na nne: kujipamba na tabia zinazosaidia kuthibiti: .................................. 24
Ya kumi na tano: Wosia wa mtu mwema ...... 25
Ya kumi na sita: Kutafakari kuhusu neema za peponi na adhabu za motoni na kukumbuka umauti:....... 25
Mawanda (Maeneo) ya Kuthibiti (Kuimarika) . 26
Ya kwanza: kuthibiti katika mitihani: ................ 26
Miongoni mwa Aina ya Mitihani: ................... 27
Ya pili: Kuthibiti katika Jihadi: ...................... 30
Ya tatu: kuthibiti katika njia (Manhaji): ......... 31
Ya tano: Kuthibiti wakati wa kifo: ................. 32
Miongoni mwa Sura za Kuthibiti: .................. 34
Bilali bin Rabaah: .......................................... 34
Ammar bin Yasir: .......................................... 35
Mus-abu bin Umair: ....................................... 36
Ummu Shariyk Ghaziyyatu binti Jabir: ............. 39